TANGAZO LA SERIKALI NA. 839 la tarehe 11/10/2024

SHERIA YA MIPANGO MIJI

(SURA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8 (1))*

AMRI YA KUPANGA ENEO LA NGULIGULI YA MWAKA, 2024

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kupanga eneo la Nguliguli ya mwaka, 2024.

Utangazaji wa Eneo la Upangaji Sura 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji kwa madhumuni ya Sheria ya Mipango Miji.

Mpango katika eneo la kwenye Jedwali

3. Mipango ya jumla na ya kina katika eneo lililoainishwa kwenye Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipango Miji na Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri ya wilaya ya Maswa.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la urasimishaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:-

"Unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MA411 yenye majira - nukta 600716MS, 9651643KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Mashariki katika uelekeo wa KZ34$^{0}$28'39"MS kwa umbali wa kilomita 4.5 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MV782 yenye majira – nukta 603255MS, 9655315KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Mashariki katika uelekeo wa KS27$^{0}$55'45MS" kwa umbali wa kilomita 4.1 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MV 781 yenye majira – nukta 606882MS, 9653397KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Magharibi katika uelekeo wa KS06$^{0}$50'34"MG kwa umbali wa kilomita 4.4 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MV711 yenye majira – nukta 606341MS, 9648936KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Magharibi katika uelekeo wa KS268$^{0}$17'58" MS kwa umbali wa kilomita 3.7 hadi kwenye alama ya

mpaka ya upimaji namba MA 410 yenye majira – nukta 602651MS, 9648817KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi katika uelekeo wa KZ225$^{0}$40'38"MG kwa umbali wa kilomita 2.8 hadi ulipoanzia."

Dodoma,
2 Oktoba, 2024

DEOGRATIUS JOHN NDEJEMBI
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*